

Kutoa Mimba

Kutoa Mimba (au 'kukomesha mimba') ni wakati mimba inatolewa kwa makusudi.

- Kutoa Mimba inaruhusiwa kisheria kule Victoria.
- Kuna aina mbili za kutoa mimba: upasuaji na kutumia dawa. Aina zote mbili ni salama na za kuaminika.
- Kule Victoria, unaweza kutoa mimba kwa kutumia dawa hadi wiki tisa za ujauzito ('ujauzito'). Unaweza kufanyiwa upasuaji wa kutoa na mimba kuanzia wiki sita za ujauzito na kuendelea.
- Kuna maeneo salama za kutolea mimba za fika hadi mita 150 karibu na kliniki za kutolea mimba huko Victoria. Hii ina maana unaweza kuingia au kuondoka kliniki bila mtu ye yeyote kujaribu kukufadhaisha.
- Daktari ambaye hataki kufanya utoaji wa mimba lazima akuelekeze kwa daktari mwingine ambaye hapingi kutoa habari za utoaji mimba na huduma.
- Matatizo makubwa ya utoaji mimba ni nadra sana. Ikiwa una wasiwasi kuhusu afya yako baada ya kutoa mimba, tafuta msaada wa matibabu.
- Ikiwa unafikiri kuhusu utoaji mimba na ungependa habari kuhusu utoaji mimba na huduma zilizopo Victoria, unaweza kutafuta: 1800myoptions.org.au au simu 1800MyOptions kwa 1800 696 784

Kulinganisha Utoaji mimba kwa kutumia dawa ama upasuaji

	Kutoa mimba kwa dawa	Kutoa mimba kwa upasuaji
Nini maana ya utaratibu hiyo?	<ul style="list-style-type: none">• Pasipo upasuaji, sawa na kuwa na mimba kutoka• Vidonge vinamezwu kwa utaratibu huu	<ul style="list-style-type: none">• Utaratibu wa upasuaji, kwa kawaida unakuwa na aina fulani ya ganzi
Je, ni ufanisi gani?	<ul style="list-style-type: none">• Asilimia 95 hadi 98 inafanikiwa• Karibu asilimia mbili hadi tano ya wanawake watahitaji vidonge vya ziada au utaratibu mdogo wa upasuaji kukamilisha utoaji mimba	<ul style="list-style-type: none">• Asilimia 98 ufanikiwa
Ni huduma za afya gani zinazotoa hiyo?	Tanzama 1800 MyOptions.org.au Njia zinajumuisha: <ul style="list-style-type: none">• Daktari wa hudama zote (GP)• Huduma za afya za jumuiya• Zahanati za kutoa mimba za binafsi na hospitali• Hospitali za umma• Kupitia 'telehealth', ambayo ni mashauriano kwa simu, na vipimo vya uthibitisho wa ujauzito kufanyika ndani ya nchi	Tanzama 1800MyOptions.org.au Njia zinajumuisha: <ul style="list-style-type: none">• Hospitali za Uma• Hospitali za ki binafsi• Zahanati za binafsi zinazo hudumu mchana

	Kutoa mimba kwa dawa	Kutoa mimba kwa upasuaji
Inafanyikia wapi?	Ushauri wa matibabu ni kwenye kliniki au kupitia telehealth (juu ya simu) na utoaji mimba unafanyika nyumbani au katika mazingira sawa.	Katika hospitali au kitengo cha upasuaji cha mchana
Muda inayao takikana?	Kufuatia kidonge cha kwanza, cha pili huchukuliwa masaa 24 hadi 48 baadaye, na utoaji mimba utafanyika saa nne hadi sita baada ya hapo, kwa wastani	Kwa kawaida ni muda wa hadi dakika 15 kwa utaratibu, pamoja na maandalizi na wakati wa kupona huchukua saa chache
Ni wakati upi wa ujamzito ndio inapaswa kufanywa	Kuanzia wakati mimba inaweza kuonekana katika ultrasound, na hadi inapofikia wiki tisa za kukua	Kwa salama na kawaida hufanyika kati ya wiki 6 hadi 12 Syo sana kwa kawaida (na ni huduma chache hutoa) wakati wa hatua za baadaye za ujauzito
Je kuna kuvujika kwa damu?	Kuvuja damu kunaweza kudumu kwa wastani wa siku 10 hadi 16	Kuvuja kwa damu hutofautiana kati ya wanawake na kunaweza kuwa uwepesi au nzito Inaweza kuendelea kwa wiki kadhaa na inaweza kuwa isivyo tarajiwa na isiyo ya kawaida
Kiasi gani cha gharama?	Wasiliana na mtoa huduma kwa habari kuhusu gharama	Wasiliana na mtoa huduma kwa habari kuhusu gharama
Ni lini unaweza kunza mpango wa uzazi	Aina nyingi za mpango wa uzazi zinaweza kuanza moja kwa moja au baada ya dawa za kutoa mimba	Aina nyingi za mpango wa uzazi zinaweza kuanza hiyo siku baada ya upasuaji wa upasuaji wa mimba

Habari zaidi

Karatasi hii ni mojawapo ya karatasi tatu kuhusu utoaji mimba kwenye Mwongozo wa Utafsiri ya Afya. Tafadhali angalia:

- Utaratibu wa kutoa mimba – kwa dawa
- Utaratibu wa kutoa mimba - upasuaji

Wapi pa kupata msaada

- [1800 my options](http://1800myoptions.vic.gov.au) Tel. [1800 696 784](tel:1800696784) mkalimani 131450
- GP wako
- [Family Planning Victoria](http://FamilyPlanningVictoria.vic.gov.au) Simu. (03) 9257 0100 au simu ya bure 1800 013 952
- Huduma ya afya ya jamii: <https://www2.health.vic.gov.au/primary-and-community-health/community-health/community-health-directory>
- Ujauzito , Uzalishaji na usaidizi wa Watoto 1800 882 436

Imeidhinishwa na kuchapishwa na Serikali ya Victoria, 1 Treasury Place, Melbourne.

© Mkoa wa Victoria, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu, Januari 2019

Ipatikana kwa <<http://healthtranslations.vic.gov.au/>>